

## **Sera ya Kupinga Ubaguzi wa Rangi**

Bodi ya Elimu na Syracuse City School District zinakataa aina zote za ubaguzi wa rangi zinazozua dhamiria, maono, thamani na malengo ya Wilaya. Madhumuni ya sera hii ni kuondoa aina zote za ubaguzi wa rangi kwenye Wilaya pamoja na sera nyingine za Bodi zinazohusika.

Bodi imeahidi kanuni zifuatazo:

1. Kuanzisha na kuendeleza jamii ya shule inayoshiriki jukumu la pamoja la kuangazia, kuondoa na kuzuia vitendo, maamuzi na matokeo yanayotokana na yanayoendeleza ubaguzi wa rangi.
2. Kuondoa desturi zisizo za usawa na kupalilia vipaji, talanta na vivutio vya kipekee vya kila mtoto ili kumaliza thamani za kutabiri za masuala ya jamii au tamaduni, kama vile rangi, tabaka, au jinsia, kwa ufanisi wa mwanafunzi.
3. Kuheshimu na kupigia debe utofauti na hali za maisha za wanajamii wote kuunga mkono dhamira, maono, thamani, malengo na shabaha za wilaya ya shule.
4. Kukiri kuwa ubaguzi wa rangi mara nyingi unahusisha aina nyingine za ubaguzi, ikiwemo lakini si tu, matabaka yale ya kulinda yaliyorejelewa katika sera ya 3420 ya Kutobagua na Kupinga Unyanyasaji.
5. Kupunguza tofauti zilizopo baina ya demografia za rangi za wanafunzi katika Wilaya na wafanyakazi ambao Wilaya inaaajiri.
6. Kuondoa tofauti baina ya makundi ya rangi katika utendaji wa masomo wa wanafunzi, ufanisi na ushiriki katika mipango ya masomo; ikiwemo: viwango vya kuhitimu, nafasi za masomo za juu au zilizochochewa, ushiriki katika kozi, shughuli za nje ya darasa, utambulisho wa elimu maalum, alama za mtihani wa wastani na viwango vya usimamishwaji.